JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Ofisi ya Rais

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Mkoa wa Mtwara

Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za afya, Ustawi wa jamii na Lishe kwa mwaka 2016

Sekretarieti ya Mkoa

S. L. P 544 Mtwara

Simu: +255 23 2333944

Fax: +255 23 2333194

e-mail: afya@pmoralg.go.tz

Website: www.mtwararhmt.go.tz

Januari, 2017

1. MIUNDOMBINU VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

4.1 Idadi ya vituo

Mkoa unavyo vituo 232 vinavyotoa huduma ya afya na kati ya hivyo 183 ni vya Serikali sawa na asilimia 82%. Vituo 16 ni vya mashirika ya dini, vituo 13 ni vya watu binafsi. Kwa mchanganuo rahisi, mkoa una hospitali 6 kati ya hizi 5 ni za Serikali na 1 ni ya shirika la dini. Vituo vya Afya vipo 21 kati ya hivyo, 14 ni vya Serikali, 4 vya mashirika ya Dini na 3 vya watu binafsi. Aidha Kuna zahanati 205, kati ya hizo 184 ni za Serikali, 13 za mashirika ya Dini, 8 za watu binafsi.

Mgawanyo wa vituo vya kutolea huduma katika Mkoa huu siyo linganifu na hasa katika wilaya ya Nanyumbu ambapo umbali mrefu kutoka kituo kimoja hadi kituo kingine pamoja na miundo mbinu mibovu hasa maeneo ya vijijini husababisha wagonjwa kusafiri umbali mrefu sana ili kupata huduma iliyo karibu ambapo inakadiriwa ni kati ya km 70 mpaka 150.

Jedwali 3: Idadi ya vituo vya kutolea huduma za Afya.

Na	Halmashauri	Hospitali	Vituo vya afya	Zahanati	Jumla
1	**Masasi DC**	1	4	41	46
2	**Masasi TC**	1	1	14	16
3	**Mtwara DC**	0	3	26	29
4	**Mtwara MC**	1	3	18	22
5	**Nanyamba TC**	0	1	24	25
6	**Nanyumbu DC**	1	2	17	20
7	**Newala DC**	0	3	22	25
8	**Newala TC**	1	1	13	15
9	**Tandahimba DC**	1	3	30	34
Jumla ya Mkoa		**6**	**21**	**205**	**232**

Hospitali zote zina jumla ya vitanda 1,159 na kati ya hivyo 859 ni vya hospitali za Serikali, sawa na asilimia 82% na 300 ni vya Hospitali ya shirika la Dini sawa na asilimia 18%. Vituo vya Afya vyote 21 kwa pamoja vina jumla ya vitanda 557, ambapo kati ya hivyo 301 ni katika vituo vya Afya vya Serikali na 256 ni katika vituo vya Afya vya mashirika ya dini.

Jedwali 4: Idadi ya vitanda kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya.

Na	Halmashauri	Idadi ya vitanda vilivyopo kwenye Hospitali	Idadi ya vitanda vilivyopo - vituo vya Afya	Jumla ya vitanda vya kupumzisha kwenye zahanati	Jumla ya vitanda vyote katika Halmashauri
1	**Masasi DC**	300	68	41	409
2	**Masasi TC**	233	25	14	272
3	**Mtwara DC**	0	83	26	109
4	**Mtwara MC**	250	72	18	340
5	**Nanyamba TC**	0	72	24	96
6	**Nanyumbu DC**	54	54	17	125
7	**Newala DC**	0	50	22	72
8	**Newala TC**	150	28	13	191
9	**Tandahimba DC**	172	105	30	307
Jumla ya Mkoa		**1,159**	**557**	**205**	**1,921**

4.2 Hali ya majengo na vifaa

Baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya ni chakavu sana kutokana na kutofanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Hata hivyo Serikali kwa kushirikiana na wananchi imekuwa ikifanya ukarabati pamoja na kujenga vituo vipya kupitia mpango wa maendeleo wa Afya ya msingi(MMAM). Kwa kifupi mkoa unahitaji zahanati 601, vituo vya Afya 191 na Hospitali 9 kulingana sera ya Afya ya kupeleka huduma ya Afya karibu na Wananchi.

Aidha upatikanaji wa madawa, vifaa Tiba na vitendanishi umeendelea kuimarika kutokana na juhudi kubwa ya Serikali ya kuboresha vituo vya huduma za Afya na mfumo wa usambazaji dawa wa moja kwa moja vituoni (Direct delivery).

Kufikia mwisho wa robo ya kwanza 2016/2017 jumla ya zahanati mpya ___ na vituo vya afya __ vipo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi(maboma)

2. VIFO VITOKANAVYO NA UZAZI

a. Idadi ya wajawazito waliojifungua kwa taarifa ni 108% ya walengwa. Kiwango hiki kinazidi asilimia 100 kwa sababu wazazi wengine wanatoka nje ya mpaka wa Tanzania (Msumbiji).

b. Kiwango cha kujifungulia katika vituo vya kutolea hudumu kimebakia kuwa asilimia 92% katika robo zote mbili.
c. Idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 51 ambapo kati ya hivyo 44 vilitokea katika vituo vya kutolea huduma na 7 vilitokea katika jamii
d. Aidha mtiririko wa vifo vya kina mama wajawazito kwa muda wa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo;
    - Mwaka 2014 idadi ya vifo 92 viliripotiwa sawa na 274/100,000
    - Mwaka 2015 idadi ya vifo 59 viliripotiwa sawa na 168/100,000
    - Mwaka 2016 idadi ya vifo 51 viliripotiwa sawa na _____/100,000

5.2 Magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

a. Viwango vya chanjo ya Surua Rubella na Pentavalent 3 vimepanda kutoka 55% na 90.2% katika robo ya nne na kufikia asilimia 78% na 99% kwa robo ya kwanza mwaka 2016/2017
b. Hatukupata mlipuko wa Surua katika mkoa ingawa wagonjwa waliokuwa na dalili zinazofanana na ugonjwa huo (Rubella) katika vijiji vilivyopo mpakani mwa wilaya ya Newala ni 40 na hakuna kifo kilichotokea.
c. Hatujapata mgonjwa wa Pepopunda ya watoto wachanga kwa zaidi ya miaka kumi sasa.

5.3 Huduma za Lishe

a. Udumavu kwa watoto chini ya miaka 5 umepungua kutoka asilimia 44 - 36.3, uzito pungufu umepungua kutoka asilimia 19 - 14.2, Upungufu wa damu mwilini umepungua kutoka asilimia 67 - 58, Idadi ya watoto waliopata Matone ya vitamini A imeongezeka kutoka asilimia 85 - 99 na idadi ya watoto waliopata dawa ya kuzuia minyoo imeongezeka kutoka asilimia 81 - 96. Pamoja na mafanikio hayo bado aslimia 3.3 ya watoto wana uzito uliozidi.
b. Tatizo la upungufu wa madini joto linaathiri 86.7% ya kaya (hawatumii chumvi yenye madini joto). Mikakati iliyopo ni kuelimisha jamii kwa kutumia Redio na mikutano na kuchukua Sampuli za chumvi kutoka katika halmashauri kwa ajili ya kupima uwepo wa madini joto

5.4 Huduma za Ustawi wa jamii

Malengo ya mkoa katika utoaji wa huduma za ustawi wa jamii ni kama ifuatavyo

a. Kuboresha utoaji wa huduma na upatikanaji wa takwimu za Ustawi wa Jamii katika Halmashauri
b. Kuimarisha mfumo wa rufaa kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto
c. Kuboresha huduma kwa watoto wa makundi maalum
d. Kushughulikia masuala ya familia, ulinzi na usalama wa mtoto
e. Kuimarisha huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu

Kazi zilizofanyika katika kipindi cha kuanzia robo ya nne ya 2015/2016 na robo ya kwanza ya 2016/2017 ni pamoja na;

a. Tulipokea na kusimamia ugawaji wa chakula cha msaada kwa kambi ya Wazee Mkaseka ulioletwa na Mhe. Mama Janeth Magufuli pamoja na misaada mingine kutoka kwa wadau.
b. Tulipokea na kusimamia ugawaji wa chakula cha msaada kwa watoto wa makundi maalum na wasiojiweza kutoka serikali ya Uturuki katika halmashauri 9 za mkoa wa Mtwara.
c. Mafunzo ya ukatili wa kijinsia na watoto kwa Halmashauri ya wilaya Mtwara yalitolewa kwa wanaohusika na utoaji huduma kwa wahanga wa ukatili, wakiwepo polisi, madaktari, watendaji wa vijiji, maafisa ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii na mashirika yasiyo ya kiserikali. Hatimae timu ya wilaya iliundwa
d. Katika kushughulikia masuala ya familia, Jumla ya kesi 170 zimepokelewa katika ofisi za Ustawi wa Jamii (mashauri ya matunzo ya watoto 91, mashauri ya ndoa 54, mashauri ya watoto wa nje ya ndoa 25) na kati ya hizo Mashauri 110 yamesuluhishwa, 26 yako mahakamani na 34 bado yanaendelea kusikilizwa
e. Kupitia mkakati wa ulinzi na usalama wa mtoto, Watoto 28 wamebakwa (kesi 20 zinaendelea mahakamani), Watoto 6 wamelawitiwa (kesi 4 zipo mahakamani), Mimba za utotoni 34 zimeweza kuripotiwa (kesi 19 zinaendelea mahakamani)
f. Klabu za ulinzi na usalama wa mtoto 52 zimeweza kuundwa katika halmashauri 7 za mkoa wa Mtwara kwa kushirikiana na shirika la **Terre des hommes Netherland**

g. Jumla ya wazee 56,869 wametambuliwa katika mkoa wa Mtwara ambapo Wazee 6,304 wamepatiwa kadi za CHF

a. Walemavu 620 wamepatiwa kadi za CHF, Walemavu wa ngozi 60 wamepata sunlight lotion, Watoto wenye ulemavu 10 walipata msaada wa baiskeli za magurudumu matatu kutoka bodi ya Ujenzi.

5.5 Huduma za udhibiti na usimamizi wa mazingira

Shughuli mbalimbali za usafi wa mazingira zimeendelea kutekelezwa kwa lengo la kuhakikisha suala la usafi wa mazingira linakua endelevu.

Kupitia kipindi hicho, tumefanikiwa kuendesha operesheni maalumu za usafi wa mazingira katika kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi ikiwa ni muendelezo wa zoezi hilo tangu kuhamasishwa na **Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika siku ya maadhimisho ya sherehe za Uhuru mwishoni **mwaka 2015**.

Kupitia operesheni hiyo maalumu, shughuli mbalimbali za usafi wa mazingira kama vile shughuli za ufagiaji, ufyekaji wa nyasi, usafishaji wa mireji ya maji ya mvua na barabara, upandaji miti, ukusanyaji na usafirishaji wa taka mpaka kwenye dampo ziliendelea kutekelezwa.

Aidha, kupitia operesheni hiyo ya usafi wa mazingira wadau mbalimbali hususani viongozi wa Serikali kuanzia ngazi ya Kijiji au Mtaa mpaka Mkoa, viongozi wa vyama vya siasa, watumishi wa umma, wanafunzi, sekta binafsi, wafanyabiashara na jamii kwa ujumla wamekua wakishiriki kikamilifu katika zoezi hilo na kusaidia hali ya usafi wa mazingira kuimarika.

a. Udhibiti wa takangumu

Kiasi kikubwa cha taka kinachozalishwa huteketezwa kwa kuchomwa moto na kufukiwa katika mashimo mafupi ambapo ni wastani wa tani 607 za taka kwa siku sawa na asilimia 70 ya taka zote zinazozalishwa huteketezwa kwa kutumia njia hizo, vilevile baadhi ya taka huzagaa katika maeneo mbalimbali kutokana na changamoto ya utupaji wa taka ovyo.

b. Udhibiti wa majitaka

Kwa upande wa udhibiti wa majitaka, tumeendelea kutekeleza kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira (National Sanitation Compaign), ambapo katika kipindi cha robo ya kwanza tu jumla ya vyoo 926 vilifanikiwa kujengwa kupitia elimu na uhamasishaji wa jamii juu ya umuhimu wa ujenzi na matumizi ya vyoo bora ilitolewa.

3. HALI YA WATUMISHI KATIKA MKOA

Mkoa una jumla ya watumishi wa afya 1,385 kati ya watumishi 3,595 sawa na asilimia 38.5 wanoaitajika kwa mujibu wa ikama ya wizara ya afya ya mwaka 2014/2018. Upungufu huu mkubwa wa rasilimali watu umeathiri kwa kiasi kikubwa zaidi katika taaluma ya Madaktari na hasa Madaktari bingwa, Wauguzi wa ngazi ya shahada na Maafisa Afya mazingira.

Jedwali 5: Idadi ya Watumishi wa kada katika Halmashauri.

HALMASHAURI	MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU
Mtwara Mikindani	299	124	175
Masasi TC	212	115	97
Mtwara DC	290	107	183
Masasi DC	750	162	588
Newala DC	305	93	212
Newala TC	344	199	145
Nanyamba TC	349	93	256
Nanyumbu DC	303	106	197
Tandahimba DC	265	112	153
Ligula Hospitali	478	274	204
JUMLA	**3,595**	**1,385**	**2,210**

Hesabu za jumla ya wagonjwa kwa kila siku (patient days) inaendelea kuongezaka, hali ya utoaji wa huduma kwa wagonjwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya imekuwa dhaifu kwa kiasi kikubwa. Kwa mtazamo wa haraka na hasa kwa kuangalia kiwango au uwezo wa hospital kulaza wagonjwa kwa mwaka (Bed occupancy rate), Wastani wa siku ambazo mgonjwa mmoja

anakaa hospitalini baada ya kulazwa (Average length of stay) na Idadi ya watu wanaotumia kitanda kimoja kwa kipindi cha mwaka mmoja (Turn over rate), inaonyesha wazi kuwa kuna mzigo wa kazi mkubwa sana kwa watumishi.

Jedwali 6: Wajumbe wa CHMT Wilaya

Halmashauri	DMO	DHS	DNO	DPharm	DLT	DHO	DDO	DSWO
Masasi DC	Yupo	Yupo	Yupo	Yupo	Yupo	Yupo	**Hayupo**	Yupo
Masasi TC	Kaimu	Yupo	Yupo	Yupo	Kaimu	Yupo	Yupo	Yupo
Mtwara DC	Kaimu	Yupo	Yupo	Yupo	Kaimu	Kaimu	Kaimu	Yupo
Mtwara MC	Yupo	Yupo	Yupo	Yupo	Yupo	Kaimu	Kaimu	Yupo
Nanyamba TC	Kaimu	Kaimu	Kaimu	Kaimu	Kaimu	Kaimu	Kaimu	Kaimu
Nanyumbu DC	Kaimu	Yupo	Yupo	Kaimu	Kaimu	Kaimu	Kaimu	Kaimu
Newala DC	Yupo	Yupo	Kaimu	Yupo	Kaimu	**Hayupo**	**Hayupo**	Yupo
Newala TC	Kaimu	Yupo	Yupo	Yupo	Kaimu	Yupo	Yupo	Yupo
Tandahimba	Yupo	Yupo	Yupo	Kaimu	Yupo	Yupo	Yupo	Yupo

4. MAFANIKIO YALIYOFIKIWA KATIKA UTEKELEZAJI WA HUDUMA ZA AFYA, USTAWI WA JAMII NA LISHE KATIKA MKOA

Miongoni mwa mafanikio kadhaa ambayo mkoa umeyapata ni pamoja na;

a. Kuimarika kwa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na hasa baada ya kuanzishwa kwa duka la dawa la Hospitali ya rufaa ya mkoa
b. Kufungwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki katika hospitali nne kati ya sita
c. Uanzishwaji wa huduma za dharura kwa kina mama wajawazito katika vituo vya afya saba kati ya tisa

d. Kuimarika kwa CHF kutoka asilimia 9% ya waliojiunga mwishoni mwa mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 28 kufikia mwishoni mwa Disemba 2016. Fedha za tele kwa tele zilizolipwa kuanzia Januari mpaka Disemba 2016 ni 80,685,000
e. Huduma za wazee zimeimarika baada ya wazee 6,304 kulipiwa CHF na Halmashauri zao kati ya wazee 56,869 waliotambuliwa.
f. Ukusanyaji wa damu salama umeimarika kwa asilimia 80% kufuatia mikakati iliyowekwa katika Halmashauri ambapo Halmashauri ya Masasi TC inafanya vizuri zaidi

5. CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio hayo zipo changamoto zinazowakabili watumishi na uongozi katika Vituo vyao vya kazi, nyingi ya changamoto hizi Uongozi wa mkoa umebaini wakati wa kutembelea halmashauri zetu, pia zimekuwa zikiwasilishwa wakati wa mikutano ya kila nusu mwaka ya wadau.

a. Kukosekana kwa dawa na vitendanishi muhimu kutoka MSD na hivyo kusababisha upungufu kwa asilimia 49.1katika vituo vya kutolea huduma
b. Uhaba wa watumishi wa kada mbalimbali kwa asilimia 61.5
c. Watumishi watoa usingizi ni wachache na wamepata mafunzo ya muda mfupi
d. Ukosefu wa magari ya kusafirishia wagonjwa (Ambullances)
e. Halmashauri tano hazina waganga wakuu kwa kipindi kirefu
f. Uchakavu wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya mkoa ya Ligula
g. Kufuatia kuhamishwa kwa watumishi wengi kwa wakati mmoja katika Hospitali ya Rufaa ya mkoa ya Ligula kumesababisha kuongezeka kwa pengo la watumishi
h. Hospitali ya Rufaa ya mkoa ya Ligula ina Madaktari bingwa wawili tu
i. Hospitali ya Rufaa ya mkoa ya Ligula inatumika kama ngazi ya msingi ya kutolea huduma za afya
j. Watumishi wengi wa Hospitali ya Ndanda kuwa nje ya payroll ya serikali na hivyo kusababisha hospitali kushindwa kuwalipa mshahara na kuamua kuwapunguza

k. Kasi ndogo ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma na nyumba za watumishi sambamba na mikakati ya MMAM

6. HITIMISHO

Mkoa utaendelea kufanyia kazi vipaumbele vya sekta ya afya, ustawi wa jamii na lishe ambavyo ni lazima kuvifikia ifikapo 2017/18

a. Kupunguza kiwango cha vifo vya watoto wachanga na wanawake vitokanavyo na uzazi kwa 20%.
b. Kuwa na mgawanyo sawa kwa 100% wa watumishi wa afya na ustawi wa jamii kwa kila Halmashauri na vituo vyote vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii
c. Kufikisha 80% ya vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vimepata hadhi ya nyota 3 kwa kila Halmashauri.
d. Kuhakikisha kuwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya vinakuwa na dawa na vitendanishi vyote muhimu kwa 100%.
e. Kuimarisha miundombinu ya Hospitali ya mkoa ili kuiwezesha kutoa Huduma za rufaa katika ngazi ya Mkoa.
f. Kupanua uwigo wa PPP kwa kushirikisha sekta binafsi kuingia katika ushirikiano na serikali katika kutoa Huduma za afya na ustawi wa jamii.
g. Kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji na tathimini (M&E) wa ukusanyaji wa takwimu na uchambuzi kwa njia ya mtandao, kuunganisha mifumo ya habari na kutoa fursa kwa wadau upatikanaji wa takwimu.